## HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KATIKA KIPINDICHA ROBO YA PILI OKTOBA HADI DESEMBA, 2017

**Mhe, Makamu Mwenyekiti**

Katika kipindi hiki kamati imefanya vikao vyake vitatu tarehe 28.11.2017, 04.01.2018 na 30.01.2018. kamati imejadili masuala mbalimbali ikiwemo suala la mapato na matumizi, taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na ukaguzi wa miradi, taarifa kutoka kwa Mkaguzi wa ndani, taarifa kutoka kitengo cha sheria, taarifa ya manunuzi, taarifa za kiutumishi pamoja na taarifa za fedha.

**Mhe, Makamu Mwenyekiti**

**Mapato na Matumizi**

Katika kipindi hiki kamati imeendelea kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ambapo kamati imeona kuwa;

- Mkakati wa kulipa deni la CHF wanalodaiwa Halmashauri uendelee. Taarifa ya ulipaji iwe inaonesha kiasi kilicholipwa na kile kilichobakia kulipwa. Dhumini hasa ni kuwawezesha Wah. Madiwani pamoja na watu wengine kuelewa vizuri kiasi halisi cha deni ambalo Halmashauri inadaiwa.
- Katika uandaaji wa taarifa za kata, kila kata iwekewe makadirio ya ukusanyaji wa mapato ili kuweza kujua hali halisi ya ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri yetu.
- Mtaalamu atakaye pokea mapato ambayo fomu yake haijasainiwa na Mhe. Diwani achukuliwe hatua.
- Kwa kuwa mawasilisho ya asilimia 20% za mwezi Julai na Semptemba yalishawasilishwa basi katika kikao kijacho kutolewe taarifa ya asilimia 20% ya mwezi Agost iliyolipwa katika kata, vilevile Asilimia 20% za kata ya Mtera na Chiporogo kwa mwezi Januari zirudushwe kwa haraka kwani mapato yake yamepanda kwa kiasi kikubwa katika mwezi Januari.

- Ushuru wa uchinjaji ni kidogo sana, Menejimenti wafanye tathimini juu ya mapato ya uchinjaji na kisha taarifa iwasilishwe katika kikao kijacho.

**Mhe, Makamu Mwenyekiti**

Ili kuhakikisha mapato ya Halmashauri yanadhibitiwa kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwa kushirikiana na Menejimenti iliunda kikosi kazi cha kufanya tathimini ya mapato ya samaki katika kata ya Chiporogo na Mtera kuanzia tarehe 19.01.2017 hadi 21.01.2018. Katika tathimni hiyo siku ya tarehe 19.01.2017 mapato yalikuwa **Tsh. 2,122,800.00** tarehe 20.01.2018 mapato yatokanayo na samaki yalikuwa ni **Tsh. 1,043,100.00,** tarehe 21.01.2018 mapato yalikuwa **Tsh 2,847,500.00** na tarehe 22.01.2018 mapato yaliyopatikana yalikuwa ni **Tsh 1,888,700.00** Hivyo kufanya jumla ya mapato yote yaliyopatikana kutokana na mapato ya samaki kwa muda wa siku tatu kufikia **Tsh 7,902,100.00.** Wakati wa tahimini changamoto mbalimbali zilibainishwa ikiwa ni pamoja na;

- Viwango vipya vya ushuru vilivyoanishwa katika sheria ndogo za mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa hazikuwa zinatozwa ipasavyo hivyo kusababisha upotevu wa mapato.
- Watoza ushuru wa mazao ya samaki hawana mizani ya kupimia mazao ya samaki hivyo hukadiria tu na hasa hukadiria kwa kadirio la chini ili kumridhisha mfanyabiashara aweze kulipa kirahisi. Mfano tenga la kg 200 la samaki wabichi lilikuwalinakadiriwa kuwa na kg 50 tu.
- Miundombinu ya barabara sio rafiki hasa kwa kipindi hiki cha mvua hazipitiki kirahisi hivyo kusababisha magari kukwama.
- Mapato mengi yanatoroshwa wakati watendaji wa Kata wanapokuja Halmashauri kuleta mapato tarehe 28 ya kila mwezi kwa kuwa huwa wanakuja na mashine zote (POS) na vitabu vyote.
- Baadhi ya watendaji hawana madaftari ya kurekodi mapato wanayokusanya kila siku.

- Wavuvi na wafanyabiashara wa samaki walisema hakujulishwa kabla kuhusu viwango vipya vya ushuru, hivyo wengi wao walipata taarifa kuanzia tarehe 19.01.2018
- Kata ya Mtera katika vijiji vyake vyote vitano hakuna Mtendaji wa kuajiriwa hivyp kufanya ufuatiliaji wa mapato kuwa mgumu.
- Kata ya Mtera haina usafiri kwa ajili ya kufuatilia na kufanya operesheni ya kukusanya mapato.
- Kuwepo kwa mgogoro katika ya Mtendaji wa kata ya Mtera na Afisa uvuvi wa Chipogoro anayesimamia mwalo wa Chamsisili.
- Watendaji wanapohama wanahama na vitabu vyote pamoja na vitendea kazi vingine na kusababisha kutokuwa na taarifa za msingi katika Kata aliyohama hasa taarifa ya mapato.
- Timu ya mapato haina mashine ya kukusanyia mapato (POS) wakati wa kufanya operesheni ya mapato.
- Kutokuwepo na ufuatiliaji wa mara kwa mara wa mapato, hivyo kusababisha wakusanyaji ushuru kuanzisha utaratibu wao mfano kupunguziana kiasi cha ushuru.

Baada ya kupitia taarifa iliyowasilishwa na timu ya tathimini wajumbe wa kamati walishauri na kuazimia yafuatayo;

a. Katika kikao kijacho kutolewe njia mbadala ya uwasilishaji wa mapato kwani hakuna ulazima wa kuweka tarehe moja tu ya uwasilishaji wa mapato ilihali mapato mengine yanapokea pindi watendaji wote wanapokuja kuwasilisha mapato yao kwa siku moja.
b. Asilimia 20% ya mapato ya samaki ya mwezi Januari yarejeshwe haraka katika kata ya Mtera na Chipogoro.
c. Mashine za kukusanyia mapato zipelekwe haraka katika sehemu za kukusanyia mapato ili kuepuka upotevu wa mapato.
d. Ili kutatua tatizo la kutokuwepo kwa Watendaji wa kuajiriwa katika vijiji vitano vya Kata ya Mtera kitu kinachopelekea ufuatiliaji wa mapato kuwa mgumu kamati

imegiza Mkurugenzi Mtendaji afutilie suala hili kwa haraka ili kuweza kudhibiti mapato katika kata ya Mtera.

e. Kuhusu suala la usafiri suala hili lichukuliwe kwa uzito na umuhimu mkubwa sana.
f. Ufanyikaji wa tathimini ya mapato uwe unafanyika pia katika minada mingine na si kwenye mapato ya samaki tu.
g. Kuwepo na malengo mahususi ya ukusanyaji wa mapato.
h. Tathimini ya mapato ifanyike tena kwa muda wa mwezi mzima katika maeneo ya minada na samaki (kuanzia tarehe 1-28.02.2018).

**Miradi ya maendeleo**

**Mhe, Makamu Mwenyekiti**

Katika kipindi hiki kamati imetembelea miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali na ambayo inatekelelezwa katika hatua mbalimbali na miradi hiyo ni pamoja na :-

- Kukagua Ujenzi wa mradi wa maji kijiji cha Kibakwe mradi wenye gharama ya Tsh. 478,929,937/= hatua iliyofikiwa ni ujenzi wa ofisi ya mradi wa COWSO imefikia hatua ya renta, vituo 9 vya maji vimejengwa bado ukamilishaji. Tanki la maji limeshamwagwa jamvi. Wakati wa ziara kamati iliweza kukutana na baadhi ya wajumbe na kubaini kuwa kuna ushirikishwaji mdogo wa wananchi juu ya ujenzi wa mradi huo , ambapo kamati iliagiza yafuatayo;
    a. Mhandisi wa Maji aende kutoa elimu kwa kuwashirikisha serikali ya kijiji, Diwani na kamati huru ya watumia maji katika kijiji cha Kibakwe ili wapate uelewa juu ya kazi zinazoendelea kufanyika na gharama za mradi zitakazotumika.
    b. Mhandisi wa Maji akafanye mchanganuo ambao utaonyesha ni kiasi gani cha fedha kitabakia baada ya kupunguza ukubwa wa tanki la maji kutoka tanki la mm75 hadi mm 50 za ujazo wa maji na taarifa hiyo iletwe kwenye kikao kijacho cha kamati ya fedha.
    c. Kamati pia iliishauri menejimenti kuwa katika uandaaji wa gharama za miradi ya COWSO wangeongeza gharama za ununuzi wa samani za ofisi.

- Kuhusu kuwezesha ujenzi na ukarabati wa miundombinu Shule ya Sekondari Chipogoro kwa gharama ya Tsh. 66,600,000/= umefikia hatua ya ukamilishaji ambapo kamati walimpongeza Mkuu wa Shule kwa niaba ya kamati kwa juhudi na hatua nzuri inayoendelea kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi.

- Kuhusu kuwezesha ujenzi wa miundombinu (ujenzi wa madarasa 3 vya madarasa, ukarabati madarasa 5, ujenzi wa matundu ya vyoo) shule ya Msingi Chinyika kwa gharama ya Tsh. 181,000,000/=kamati hawakuweza kufika kwakuwa njia haipitiki katika kipindi cha masika.

- Ukaguzi kuhusu uwezeshaji wa ujenzi wa miundombinu katika kituo cha Afya Mima, kwa gharama ya Tsh. 500,000,000/=, ujenzi wa nyumba 1 ya mganga na maabara imefika hatua ya ukamilishaji, ujenzi wa chumba cha upasuaji umefikia hatua ya upauaji, ujenzi wa msingi wa wodi 1 ya watoto na wodi 1 wazazi, upimaji wa jengo la kuhifadhia maiti unaendelea. Kamati pia imempongeza mwenyekiti wa kijiji kwa juhudi walizofanya za kuanzisha ujenzi wa nyumba 1 ya mganga ambayo imefikia hatua kukamilisha ujenzi wa msingi.

- Kamati pia ilikagua ujenzi wa mradi wa maji Mima wenye gharama ya Tsh.478, 604,719. Ujenzi wa vituo vya maji upo katika hatua ya awali. Kamati iliiagiza Menejimenti kuwa mradi huo uendelee.

**Mhe, Makamu Mwenyekiti**

**Hoja za Mkaguzi wa ndani**

Katika kipindi hiki kamati imepokea taarifa utekelezaji kutoka kwa Mkaguzi wa Ndani ambapo hoja mbalimbali zimehojiwa. Kamati imeungana na Mkaguzi wa Ndani kuitaka Menejimenti itekeleze yale yote yaliyohojiwa ili hoja ziweze kufungwa.

**Mhe, Makamu Mwenyekiti**
**Manunuzi**
Katika kipindi hiki Kamati pia imepokea taarifa kutoka kitengo cha manunuzi ambapo katika robo hii kumefanyika manunuzi ya kawaida (vifaa na huduma) wenye thamani ya Tsh 4,329,597,985.13

**Mhe, Makamu Mwenyekiti**
**Kitengo cha sheria**
Kamati imepokea taarifa ya idadi ya kesi mbalimbali ambazo zipo mahakamani na ambazo zimetolewa maamuzi. Ambapo pamoja na kesi hizo kamati imeshauri kuwa mwanasheria awezeshwe anapoenda kusikiliza kesi dhidi ya Halmashauri.

**Mhe, Makamu Mwenyekiti**
Pamoja na taarifa hii nimeambatanisha viambatanisho vya taarifa ya Mapato na matumizi kuishia mwezi Desemba, 2017 pamoja na taarifa ya miradi ya maendeleo.

**Mhe, Makamu Mwenyekiti**
Naomba Baraza lako tukufu liweze kuridhia mapendekezo na maazimio yaliyoafikiwa na Kamati.

Nawasilisha

………………………
Mhe, Donati .S. Nghwenzi
**MWENYEKITI WA KAMATI**
**KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO**